



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
WILAYA YA MBULU

Simu Na. 027-2533019  
Simu Na. 027-2533036  
Unapojibu tafadhali taja:-

Wilaya ya Mbulu,  
S.L.P.1,  
MBULU.

Karita. Na. AD. 59/200/0172

16.07.2022

**TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI**

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu anapenda kuwaarifu Waombaji wote walioomba kazi ya Ajira za Muda ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 zilizotangwa kupitia tangazo la tarehe 05/05/2022 hadi tarehe 19/05/2022 kuwa Usaili unatarajiwa kufanyika tarehe **19/07/2022 hadi 20/07/2022** katika Maeneo yaliyoainishwa kweye Jedwali lililopo hapo chini kuanzia saa **1.30 asubuhi**.

Waombaji watakaofaulu Usaili, majina yao yatabandikwa katika Mbao za Matangazo za Halmashauri zao na Kata husika.

Ratiba ya Usaili kwa Nafasi zilizotangazwa itakuwa kama ifuatavyo:-

NA.	NAFASI	TAREHE YA USAILI	NGAZI YA USAILI	MAHALI
1.	Karani wa Sensa	19 – 20 Julai, 2022	Kata	Makao Makuu ya Kata
2.	Msimamizi wa Maudhui	19 – 20 Julai, 2022	Kata	Makao Makuu ya Kata
3.	Msimamizi wa TEHAMA	19 – 20 Julai, 2022	Wilaya	Makao Makuu ya Halmashauri
4.	Matokeo ya Usaili katika kila Kata yatapitiwa na kuidhinishwa na Kamati ya Sensa Wilaya	21 – 22 Julai, 2022	Wilaya	Ofisi ya Mkuu wa Wilaya

Aidha, Waombaji walioitwa kwenye Usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- Wafike katika Eneo la Usaili kulingana na Nafasi walizoomba.
- Kila Mwombaji atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi.
- Kila Mwombaji anapaswa kuwa na Kitambulisho kwa ajili ya Utambuzi. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na: Kitambulisho cha mkazi, kitambulisho cha Mpiga kura, Kitambulisho cha Uraia au Hati ya kusafiria.
- Mwombaji ambaye hatafika na nyaraka zilizoainishwa hataruhusiwa kufanya usaili.
- Mwombaji ambaye hatafika katika Usaili atakuwa amepoteza nafasi yake.
- Waombaji ambao majina yao hayajaonekana kwenye orodha iliyoambatishwa pamoja na tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo hitajika.



Sezarla V. Makota  
**MKUU WA WILAYA  
MBULU**

**Nakala:** Mbao za Matangazo

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu – Kwa utekelezaji

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu – Kwa utekelezaji



**Sensa kwa Maendeleo; Jiandae Kuhesabiwa**